# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI

ISSN 2507 - 797 Toleo Maalum No 3 2023/2024

## TUMEJIVUNIA MABADILIKO MAKUBWA

2023
KARIBU
2024



*Wekeza katika Uchumi wa BULUU*



**TUNABORESHA MIUNDOMBINU YA ELIMU, AFYA KILA KATA**

**MHARIRI MKUU**
**Aquilinus Shuduki**

**MHARIRI MSAIDIZI**
**Beatha Singano**

**WAPIGA PICHA**
**Kaunga Maulid**
**Filbert Odilo**

**MSANIFU JARIDA**
**Jamila Mdemu**

**WAANDISHI**
**Jamila Mdemu**
**Athuman Ntafumila**

**JARIDA HILI LIMETOLEWA NA**


**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni**
**S.L.P KINONDONI, 31902 DSM**
**SIMU: +255222170173**
**BARUA PEPEP: md@kinondonimc.go.tz**




# TAHARIRI

## KWA HERI 2023, KARIBU 2024

Tunapouaga mwaka 2023 na kuukaribisha mwaka 2024, Manispaa ya Kinondoni inapenda kutoa salama za heri ya Mwaka Mpya kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri yaMuungano wa Tanzania, Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Viongozi wote wa ngazi mbalimbali na Watanzania popote walipo.

Manispaa ya Kinondoni inaungalia mwaka 2023 kwa kutafakari mafanikio makubwa yaliyopatikana katika ubopreshaji wa miundombinu ya sekta za utoaji huduma za jamii, uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuendelea kukamilisha na kuazisha miradi mbalimbali.

Licha ya kwamba kwa kalenda ya Serikali ya mwaka 2023/2024 ndiyo tunaanza nusu mwaka, hata hivyo katika kipindi cha mwaka mzima wa 2023, Manispaa ilifanikiwa kwa kisi kikubwa kuboresha miundombinu katika sekta za Afya ambapo tumeumaliza mwaka 2023 tukiwa na vituo 35 vya kutolea huduma za afya, Vituo hivi ni Zahanati 25, vituo vya Afya 9 na Hospitali moja ya Wilaya iliyopo Mabwepande.

Hakika tumehakikisha tunarahisisha huduma ya kusafirisha wagonjwa kwa kununua magari mawili ya wagonjwa.

Katika kipindi hicho Manispaa pia imeweza kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Bus cha Kisasa kilichopo Mwenge, ujenzi wa kituo hicho, kikiwa ni kitovu cha uwekezaji ndani ya Manispaa huku kitachangia fursa nyingi za uwekezaji na ajira kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ndani na eneo hilo.

Manispaa pia, katika Mwaka huu wa 2023 iliweza kuendelea na ujenzi wa uwanja wake wa Mpira uliopo Mwenge. kukamilika kwa uwanja huu wa mpira kutanchangia mabadiliko makubwa katika sekta ya michezo hususani soka.

Ikumbukwe kuwa Kinondoni ndiye Manispaa yenye Timu ya Mpira KMC FC na kuwa Manispaa inayomiliki kiwanja chake.

Katika sekta ya Elimu Msingi awali na Sekondari, Manispaa imeendelea kuboresha miundombinu yake kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa, madawati, maabara, kiasi cha zaidi ya Shilingi Bilioni 5.1 zimetumika katika uboreshaji wa miundombinu ya elimu. Tunatarajia ifikapo Januari, 2024 Kata ya Tandale itakuwa imehitimisha kuwa na shule yake ya Sekondari ambapo zitatimia Shule 35 za Sekondari.

Tumefunga mwaka 2023 kwa kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia vikundi 4,426 vya wajasiriamali. Jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 17.8.imeshatolewa kwa vikundi hivyo.

Tunapoingia mwaka 2024, tunazidi kuuahidi umma wa wana Kinondoni kuwa, Manispaa yenu itaongeza ufanisi katika uboreshaji wa miindombinu ya huduma za kijamii na kuchumi. Kwa upande mwingine, tunazidi kuwahimiza wananchi wote na wafanyabiashara kuendelea kulipia tozo mbalimbali za Manispaa.

Ulipaji wa tozo hizo zikiwemo za mabango, majengo na nyinginezo zitaiongezea Manispaa nguvu ya kuendelea kuboresha miundombinu ya Elimu, Afya, Maendeleo ya Jamii na hata Uwekezaji.

Karibu Mwaka 2024, Mwaka wenye matarajio Makubwa kwa Manispaa ya Kinondoni.



# MAJUKWAA YA WANAWAKE YAWAKWAMUA KIFIKRA NA KIUCHUMI

**Na**
**JAMILA MDEMU**

Kupitia zinduzi za majukwaa zilizofanyika katika Kata za Manispaa ya Kinondoni zimepelekea wanawake kujikwamua kiuchumi na kifikra kwa kupata connection na elimu ya kutosha dhidi ya ujasiriamali na biashara kwa ujumla.

Uanzishwaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi umeleta mabadiliko kwa wanawake hususani kujikwamua kifikra kwa kupata elimu itolewayo mara kwa mara kuhusiana na fursa zitolewazo kwa wanawake.

Lengo la kuanzishwa kwa majukwaa hayo ni pamoja kuwaunganisha wanawake kutoka sehemu mbalimbali, kupeana elimu kuhusiana na ujasiriamali, kupeana fursa mbalimbali, kupeana ujuzi wa namna ya kutafuta masoko ya bidhaa na kujua misingi ya namna ya kufanya biashara.

Akizungumza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Albert Chalamila katika Uzinduzi wa Majukwaa hayo Wilaya ya Kinondoni alisema, atakuwa bega kwa bega kwa kufuatilia Majukwaa hayo ili yaendele kuleta tija.

Alitoa kauli hiyo katika uzinduzi huo alipofugua Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ngazi ya Wilaya ya Kinondoni yaliyofanyika katika Viwanja vya Biafra Manispaa ya Kinondoni.

Ufunguzi huo ulitanguliwa na maonesho ya Wajasiriamali wanawake kutoka Kata zote za Manispaa ya Kinondoni ambapo walipata fursa za kuonesha bidhaa mbalimbali.

Alisema, Mwanamke akishika rungu la uchumi, familia zote




***Mbunge wa Jimbo la Kinondoni Mhe. Abbas Tarimba (katikati) akiongoza zoezi la uzinduzi wa Majukwaa ya Wanawake uliofanyika katika Kata ya Kijitonyama, Wilaya ya Kinondoni.***

zitakomboka kwani mwanamke akiwezeshwa anaweza kuleta mapinduzi mkubwa sana kiuchumi.

Aidha, aliwatka Wanawake kuendeleza upendo, umoja na mshikamano ili kujenga jeshi moja lenye lengo la kuleta maendeleo katika nchi.

Vilevile, aliwapongeza wanawake na washiriki wa maonesho hayo kwa kujenga mtandao mkubwa uliowawezesha kuonyesha bidhaa zao zinazosaidia kujikwamua kiuchumi, “Kataeni dhana ya utegemezi ili muweze kusimama na kujikwamua kiuchumi”.

Akiongea Mbunge wa Jimbo la Kinondoni Mheshimiwa Abbas Tarimba katika Uzunduzi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi aliwataka wanawake kuibua fursa zenye tija na manufaa ili kukua na kuwanufaisha katika adhima ya kuinuka kiuchumi. “Tumieni majukwaa haya kuibua fursa zenye tija na zinazotekelezeka kwa kuanza na fursa ndogo na mwisho kuwa kubwa”.

Akizungumza Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Taifa Bi Fatma Kange aliwataka wanawake wajasiriamali kutumia jukwaa la teknolojia kutangaza biashara zao ndani na nje ya Nchi.

Bi. Fatma aliongeza kuwa, biashara wanazofanya wanawake wajasiriamali zinaweza kufanyika kwa weledi na mafanikio ikiwa watatumia maendeleo ya teknolojia iliyopo. “Wanawake tutumie jukwaa la teknolojia kutafuta mtandao wa kuuza bidhaa zetu, tusitumie jukwaa hilo la teknolojia kupiga umbea. “ Aliongeza Bi Fatma Kange.

Vilevile, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bw. Jabir Chilumba alisema, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetenga kiasi cha shilingi Bilioni 5.2 kwa ajili ya mikopo ya asilimia 10 kwa wajasiriamali kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

***Inaendelea Kutoka Uk... 3***

Aliwataka wajasriamali hao kuendelea na uzalishaji wa bidhaa kutokana na serikali kuwaunga mkono na kwamba " Manispaa ya KInindoni itaendelea kuwashika mkono na kuwatafutia masoko ndani ya nje ya Nchi.

Pia Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam mheshimiwa Janeth Mahawanga alitoa majiko 20 yanayotumia gesi kwa Mamalishe ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa Jukwaa la kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Majiko hayo yaliwawezesha Mamalishe hao kuachana na matumizi ya kuni na mkaa katika shughuli zao za kujiafutia kipato.

Pia, Diwani wa Mbezi juu Mheshimiwa Anna Lukindo alisema, "Jukwaa lina mlengo mzuri, kikubwa ni kujipanga na kufikia malengo yaliyowekwa ili kuleta tija". Akaongeza kuwa, kuwepo na kituo cha kukutanisha majukwaa yote kwa ajili ya kutatua changamoto zao.

Matarajio ya uwepo wa majukwa haya ni pamoja na kutatua changamoto ya ajira, kuzalisha bidhaa bora, kukuza masoko, kuwakutanisha wanawake mbalimbali na kuanzisha maonesho ya bidhaa zitakazotengenezwa na wajasiriamali.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Mbezi Juu Bi. Sume Seiph amesema, zinduzi za majukwaa haya zimeleta muamko kwa wanawake kwa kupata elimu pamoja na faida za uwepo wa majukwaa hayo.

Ameongeza kuwa, "muitikio wa wanawake ni mkubwa kutokana na sapoti inayotolewa na viongozi wa Manispaa ya Kinondoni sambamba na elimu itolewayo".







***Picha mbalimbali zikionesha uzinduzi wa Majukwaa ya Wanawake katika Kata zote za Manispaa ya Kinondoni kwa mwaka 2023.***






# 2024 TANDALE KUWA NA SEKONDARI





**Na**
**ATHUMAN NTAFUMILA**

Wananchi na Wakazi wa Kata ya Tandale wameishukuru Serikali kwa ujenzi na ukarabati wa Shule ya Awali, Msingi na Sekondari ya Mhalitani.

Awali Kata ya Tandale ilikuwa ni Kata pekee kwa Kata za Wilaya ya Kinondoni ambayo haikuwa na Shule ya Sekondari, hali hii ilionekana kuwasumbua Watoto na Wazazi wengi kwa kufuata huduma hiyo umbali mrefu.

Diwani wa Kata ya Tandale Mhe. Abdallah Said, amesema kuwa tatizo la Kata ya Tandale kukosa Shule ya Sekondari kwa mda mrefu limetatuliwa kwa kishindo, kwasababu Shule inayotarajiwa itakuwa ya mfano kwa Nchi nzima.

"Nitumie fursa hii kuishukuru Serikali ya awamu ya sita na Uongozi wa Wilaya ya Kinondoni kwa kujali na kutatua matatizo ya Wananchi" ameongeza Mhe Diwani.

Kwa Upande wake Afisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Bw. Mtondi Nyamhanga amesema kuwa, tatizo la kukosa Shule ya Sekondari kwa Kata ya Tandale linatokana na ufinyu wa maeneo.

Bw. Nyamhanga amesema kuwa, namna ya kumaliza tatizo hilo Manispaa kwa kushirikiana na Serikali wameibadilisha iliyokuwa Shule ya Msingi Mhalitani kuwa Shule ya Awali, Msingi na Sekondari Mhalitani.

Mabadiliko hayo yameenda sambamba na ukarabati wa Madarasa 11 ambayo Januari, 2024 yatapokea wanafunzi wa Awali, Darasa la kwanza na kidato Cha kwanza, Wakati huo ujenzi wa wa jengo la Ghorofa nne utakaogharimu Bil 3.8 ukiwa mbioni kuanza.

Bw. Nyamhanga amesema kuwa wanafunzi waliokuwa wanasoma Shule ya Msingi Mhalitani wamehamishiwa katika Shule ya Msingi Tandale Magharibi na Hekima ambapo kwa ujumla wao walikuwa Wanafunzi 750.

Shule ya Awali, Msingi na Sekondari Mhalitani itakuwa Mojawapo ya Shule za mwanzo kabisa kuanza kutumia Mtaala mpya wa Sera ya Elimu ulioanzishwa mwaka huu, ambao unawataka Wanafunzi wa Shule za Msingi kuishia Darasa la sita na kujiunga na kidato Cha kwanza.

Mhidin Said, Mkazi wa Kata ya Tandale amesema kilio Cha Wakazi wa Tandale, kuhusiana na kadhia waliyokuwa wanaipata Watoto wao kwa kusafiri umbali mrefu kufuata huduma ya Elimu kimefika mwisho.

# WATOTO CHINI YA MIAKA MITANO WASAJILIWA

**Na JAMILA MDEMU**



Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imezindua Kampeni ya Usajili wa watoto kuanzia miaka mitano kushuka chini kwa lengo la kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto ambao walikuwa hawajasajiliwa.

Zoezi hilo linaendelea kufanyika katika Vituo vya Afya, Hospitali, Zahanati na katika Ofisi za Kata za Manispaa ya Kinondoni ambapo litafanyika mpaka tarehe 8 Machi, 2024 na baada ya hapo zoezi litaendelea kwa watoto wenye umri wa siku 90 watakaopewa huduma katika eneo husika la Manispaa ya Kinondoni.

Katika kufikia malengo hayo, Manispaa ya Kinondoni imepaga kusajili watoto 51, 774 na mpaka sasa watoto waliosajiliwa ni 15,444 na kuingizwa katika mfumo.

Manispaa ya Kinodnoni imejipanga kuwafikia wananchi kwa kuwapa matangazo ya mtaa kwa mtaa katika Kata mbalimbali ndani ya Manispaa ya Kinondoni, kujenga uelewa kwenye mkusanyiko wa watu sambamba na kupita nyumba kwa nyumba ili kutoa huduma za usajili huo.

Vile vile MAnispa ya KInondoni imejipanga kutoa taarifa kwa viongozi wa nyumba za ibada ili kuhakikisha taarifa zinafikia jamii kwa kiasi kikubwa.

Aidha, Afisa Ustawi wa Jamii Bi. Sturda Nselu amesema,"huduma hii ya usajili na upatikanaji wa cheti kwa watoto wa miaka mitano ni bure na cheti hicho kitatambulika sehemu yoyote".

Ameongeza kuwa, mapokeo ya wananchi ni makubwa kutokana na taarifa zipatikanazo kupitia matangazo sambamba na elimu ipatikanayo katika clinic zitolewazo katika vituo vya afya vya Manispaa ya Kinondoni.

# MAANDALIZI YA UZINDUZI WA KITUO KIPYA CHA MABASI MWENGE



# JARIDA LA MANISPAA YA
# KINONDONI








*Jarida la Manispaa ya Kinondoni 2023/2024*
*www.kinondonimc.go.tz*